504007

KENYA NATIONAL ASSESSMENT SERIES

# UTABIRI WA PILI - 20/21

504

# - KISWAHILI -

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Saa 1 Dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:-

   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mithani (yaani nambari ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa katarasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano:**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **Kutoka swali 16-30, chagua jibu sahihi.**

20. Kutokana na kitenzi hama tunapata nomino
    A. hamia
    B. hama hama
    C. mhamiaji
    D. mahame

    Jibu sahihi ni **D**.

    **Katika karatasi ya majibu**

    **18.** [A] [B] [C] [D]   **19.** [A] [B] [C] [D]   **20.** [A] [B] [C] [~~D~~]   **21.** [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **20**, kisanduku herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

*© Hero Educational Publishing House, 2021*

909504

*For enquiries call, 0722 424273 / 0111 363432*

**FUNGUA KURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, chagua jawabu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Kandamiza hakujua thamani ___**1**____ watoto ____**2**___ siku moja ___**3**_____na ulimwengu. Alizoea kuwatumikisha watoto wadogo kwa ___**4**____ kuwaajiri watu wazima asije akajiumiza kwa kuwalipa mishahara mikubwa. Siku moja mwanawe mmoja ambaye ___**5**_____ kuyamudu masomo aliamua kuondoka nyumbani bila kuaga. Kandamiza alipogundua kuwa mwanawe ____**6**____ mjini alihuzunika mno. Moyoni kandamiza alijua kuwa mtoto huyo ___**7**_____jinsi yeye alivyowafanya watoto wa wengine.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. wa | B. za | C. la | D. ya |
| **2.** | A. sasa | B. hadi | C. tangu | D. lau |
| **3.** | A. alipofunzwa | B. alikofunzwa | C. aliofunzwa | D. aliyefunzwa |
| **4.** | A. kuchelewa | B. kupenda | C. kuchelea | D. kupendelea |
| **5.** | A. hawezi | B. hakuweza | C. hataweza | D. hajaweza |
| **6.** | A. ametoroka | B. ametoroshwa | C. ametorokea | D. ametorosha |
| **7.** | A. angetesa | B. angemtesa | C. angewatesa | D. angeteswa |

Taifa lolote ___**8**____ wananchi wenye afya. Magonjwa _____**9**____nchi hasara ___**10**_____ ___**11**_____ pia huwa mzigo mzito kwa mtu binafsi ___**12**___ ya magonjwa hutokana na ____**13**_____ usafi. ___**14**___ huweza kuzuiwa iwapo wananchi wataitikia wito wa kunadhifisha makazi ___**15**____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | A. huhitaji | B. hahitaji | C. yahitaji | D. lihitaji |
| **9.** | A. hailetei | B. haileti | C. hayaileti | D. hayailetei |
| **10.** | A. ajabu | B. kamwe | C. tu | D. naam |
| **11.** | A. bali | B. mbali | C. na | D. ijapokuwa |
| **12.** | A. baina | B. baadhi | C. kati | D. zaidi |
| **13.** | A. kutodumisha | B. kutodumu | C. kudumisha | D. kudumu |
| **14.** | A. hii | B. hizi | C. hiyo | D. haya |
| **15.** | A. lao | B. yao | C. zao | D. wao |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** Chagua jibu linaloonyesha aina za mashairi pekee

A. Tarbia, takhmisa

B. Tarbia, mizani

C. Vina, takhmisa

D. Takkhmisa, ubeti

**17.** Kanusha kwa usahihi: **Nyumba hiyo ikijengwa vizuri tutahamia huko**

A. Nyumba hiyo ikijengwa vibaya hatutahamia huko

B. Nyumba hiyo ikibomolewa vibaya hatutahamia huko

C. Nyumba hiyo isipojengwa vizuri hatutahamia huko

D. Nyumba hiyo isipojengwa vibaya hatutahamia huko

**18.** Usemi wa taarifa wa, "**mtavinunua vitabu vyenu kesho Jumatatu,**" mwalimu alituambia.

A. Mwalimu alituambia kwamba tungevinunua vitabu chetu siku iliyofuata jumatatu

B. Mwalimu alituambia kuwa tutavinunua vitabu vyetu siku hiyo ya jumatatu.

C. Mwalimu alituambia kwamba tungevinunua vitabu vyetu siku iliyofuata ya jumatatu.

D. Mwalimu alitushauri kuvinunua vitabu vyetu siku hiyo iliyofuata.

**19.** Kutokana na nomino **ushujaa** tunapata kitenzi.

A. Shujaa

B. Shajiisha

C. Mshujaa

D. Shupavu

**20.** Chuma ameolewa na Hamisi. Hamisi ana dada aitwaye Hadija. Je, Hadija na Chuma wataitanaje?

A. Mwamu

B. Wifi

C. Mpwa

D. Mavyaa

**21.** Andika sentensi zifuatazo katika kauli ya kutendewa.

**Juma aliosha gari jana. Gari lilikuwa kwa jabali.**

A. Juma alioshewa gari na jabali jana

B. Gari lilioshwa na juma jana kwa jabali

C. Gari lilioshewa kwa jabali na juma jana

D. Jabali alioshewa gari na juma jana

**22.** Chagua jawabu lililo na sauti ghuna pekee.

A. m, f, g, th

B. v, z, w, dh

C. ch, s, d, t

D. n, gh, h, k

**23.** Tambua maneno yaliyopigiwa kistari katika sentensi ifuatayo:

**Mwalimu aliwafundisha wanafunzi <u>wengi darasani</u>.**

A. Kielezi, kiwakilishi

B. Kivumishi, kihusishi

C. Kiwakilishi, kihusishi

D. Kivumishi, kielezi

**24.** Malipo kwa mtu aliyekiokota kitu kilichopotea huitwa ______ ilhali ya mtu aliyestaafu huitwa ______.

A. Kiangazamacho, kiinuamgongo
B. Kiokozi, karisaji
C. Fungule, marupurupu
D. Mrabaha, penisheni

**25.** Ni sentensi gani iliyotumia **kwa** kuonyesha jinsi ya kufanya jambo.

A. Mwalimu anandika ubaoni kwa chaki
B. Tulishinda mabao mawili kwa matatu katika mechi hiyo.
C. Ni vyema kuwaamkua wakuu wetu kwa heshima na taadhima
D. Mwanariadha alituzwa kwa weledi wake.

**26.** Tambua sentensi isiyo sahihi kulingana na neno panda.

A. Bei ya bidhaa kupungua
B. Sehemu ya mbele ya kichwa
C. Sehemu matawi ya mti yanapokutana
D. Fukia mbegu ardhini

**27.** Chagua kundi lenye vielezi pekee

A. maadam, kefle, hamadi, lau
B. vizuri, sana, kijeshi,ovyo
C. safi, tifu, iwapo, bali
D. nje ya, labda, ingawa, hata

**28.** Tegua kitendawili:
**Nikitoka anifuata nikiingia apotea**

A. kioo
B. jua
C. kivuli
D. mtoto

**29.** Chagua sentensi ambayo si sahihi kati ya zifuatazo.

A. Mwalimu wao ni mjuzi kwa mujibu wa matokeo ya mtihani
B. Wapo watoto wanaoishi mitaani kwa mighairi ya kukosa makazi
C. Mgeni alifika mapema licha ya mvua kubwa kunyesha jana
D. Wanafunzi wengi wangepita mtihani lau wangesoma kwa bidii.

**30.** Watu wengi wanasisitiziwa kuyatunza mazingira ili wasiathirike baadaye. Ni methali gani iliyolingana na maelezo haya.

A. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe
B. Rasharasha ndio mwanzo wa mvua
C. Maji ukiyavulia nguo yaoge.
D. Kambale mkunje angali mbichi

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.***

Katika kijiji kimoja kijulikanacho kama Mamboleo, kuliondokea kijana mmoja ambaye Mungu alimtunukia bongo. Kijana huyu alijulikana kwajina Idili. Darasani alikuwa hawezekani. Akasoma kwa bidii ya mchwa hadi kafika chuo kikuu na kuvunja rekodi kwa kukwangura alama nzuri ajabu. Baadaye akaoa **mke kufu** yake kujikopoa watoto ambao nao waliziandama nyayo za wazazi wao.

Jambo lililokuwa linaikera familia ya kina Idili ni ukosefu wa kuwajibika kwa ndugu zake. Kaka zake walikuwa wazembe na visu butu shuleni. Kila waliposhauriwa kuwa wasome vyema kama ndugu yao Idili, walipuuza na kucheka, wakashindwa hata kuchungulia vile vidato vya sekondari vifunguavyo vijana macho na akili zaidi. Tabia zao zikazorota, wakawa wanapiga mtindi na kuzurura tu.

Ingawa tabia za ndugu hawa ziliendelea kuwa mbaya, Idili hakukata tamaa kabisa mara kwa mara aliwaita na kuwashika sikio na kuwapa mawaidha. Alijitolea kuwalipia ada za kwenda kusomea masomo ya ngubaru ili angalau waweze kujishikiza katika sekta ya 'jua kali' lakini wapi! Walianza masomo na kuyaachia njiani.

Wazazi walipokaribia kuwapungia mikono wana wao humu duniani, waliwaita pamoja na kuwapa wosia na hata kuwapa urithi wa mashamba. Idili akawaambia ndugu zake kuwa kwa kuwa anao uwezo yeye atawaachia hayo mashamba ili wayalime na kujiinua kiuchumi. Wazee wakafurahi kuona kuwa Idili alijali maslahi ya wadogo zake.

Baada ya vifo vya wazazi wao, wadogo hao hawakuchelea **kuipiga mali shoka** mara moja. Idili aliwaonya lakini aliambulia nunge. Maonyo hayo yote yaliingilia sikio moja na kutokea lile jingine, huku yakipurukia hewani.

Siku moja ajali mbaya ya barabarani ikaamua kuyakatisha maisha mema ya Idili na mkewe. **Huzuni iliwakumbatia wana wao lakini majirani na marafiki wakaingilia shughuli za mazishi na kuzimaliza**. Wakaanza kuwatunza watoto ambao wakati huo walikuwa wakimalizia elimu ya shule za msingi.

Nduguze Idili walikuwa wakifikiria wamepata vya bwerere na kujiona wakifaidi mali ya Idili na mkewe kama tu ile ya wazazi. Hata hivyo, juhudi si pato. Waliyoyataka hayakuwa. Marafiki wa Idili waliyatilia guu matendo ya ndugu hawa ambao walikuwa wameanza kuinyemelea mali ya Idili. Walijaribu kwa udi na uvumba kuzuia dhuluma hii na walipoona mambo yatachacha wakawasaidia watoto kwenda katika korti ya watoto kutetea haki zao. Ami za watoto hawa wakashtakiwa kwa madai ya jaribio la unyang'anyi wa urithi. Uzuri ukawa Idili na mkewe nao walikuwa wameandikisha urithi wa watoto wao na kumwachia wakili. Wakili aliwaonyesha nduguze Idili hati hizo wakawa hawajui pa kuziweka nyuso zao. Wakajua kuwa watoto nao wana haki ya kurithi. Pia walielewa kwamba kusoma ni kuzuri. Kama wangalisoma vyema wangalikuwa na vyao lakini walibaki kuwa hohehahe wasio na mbele wala nyuma.wakawa wanategemea cha ndugu ambacho **hakikuwasitiri**.

**31.** Idili alithibitisha werevu wake kwa

A. Kupita mitihani yote, kuonya ndugu, kutii wazazi, kuacha urithi wake.

B. Kupita mitihani yote, kupenda majirani, kuwaachia wanawe urithi chini ya wakili.

C. Kupita mitihani yote, kuonya ndugu, kuwaachia wanawe urithi chini ya wakili.

D. Kupita mitihani yote, kupenda ndugu, kuwaachia urithi chini ya wakili.

**32.** Wazazi wa Idili walikuwa na busara kwani

A. Waliwaachia wana wao urithi

B. Walikuwa na maonyo mengi

C. Waliwaonya wana wao wakaskia

D. Waliwapa wasia wana wao wamtii Idili

**33.** Ndugu wa Idili waliposhauriwa wasome walicheka kwa sababu

A. Hawakuona haja ya masomo

B. Walitarajia kufaidi mali ya ndugu yao

C. Idili hakuwa tajiri ijapokuwa alisoma

D. Walishindwa kuendelea na masomo

**34.** Nduguze Idili

A. Walisomea kazi za ufundi

B. Waliachia masomo shule ya msingi

C. Walisoma ngubaru wakakosa kupata kazi

D. Walifundishwa kazi za jua kali wakashindwa

**35.** Maana ya **mke kufu** ni

A. Mke wa jamii yake

B. Mke aliyelingana naye

C. Mke wa kijiji chake

D. Mke aliyesoma naye

**36.** Baada ya vifo vya wazazi wao, nduguze Idili

A. Walidhani watafaidi mali

B. Waligawiwa mali wengine wakaifuja

C. Walimnyima Idili urithi wote

D. Walianza kuifuja mali mara moja

**37.** "*Huzuni iliwakumba wana wao lakini majirani na marafiki wakaingilia shughuli za mazishi na kuzimaliza*". Methali inayolingana na maneno haya ni?

A. Damu ni nzito kuliko maji

B. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

C. Kenda fumbata ni bora kuliko kumi nenda rudi.

D. Ndugu mui heri kuwa naye

**38.** Neno hakikuwasitiri kama lilivyotumika katika kifungu linamaanisha

A. Hakikuwakamilisha

B. Hakikuwatamanisha

C. Hakikuwafunikia aibu

D. Hakikuwatosheleza

**39.** Maneno kupiga mali shoka yana maana gani kulingana na kifungu?

A. Kutumia mali vibaya

B. Kugawanya mali yote

C. Kuhifadhi mali yote

D. Kupiga mali bei

**40.** Haki za watoto zilitimizwa kwa

A. Kusomeshwa, kuonywa, kusaidiwa, kuishi na ndugu wakiwa mayatima

B. Kulindiwa urithi wao na ndugu, kugawiwa urithi na kusaidiwa na majirani

C. Kusomeshwa, kusaidiwa walipofiwa, kupewa urithi na kuelekezwa kushtaki maonevu

D. Kutomruhusu yeyote kuwanyang'anya mali, kuelekezwa kwa mashtaka na kuruhusiwa kuuza mali.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Uamuzi uliofanywa na serikali wa kuhimiza watoto wote warudi shuleni ni jambo mwafaka. Watoto walifurika furifuri shuleni ili kusajiliwa. Wale waliokuwa wakirandaranda mitaani walifuatilizwa himahima na kupelekwa shuleni. Waliokuwa wakubwa kiumri walipelekwa kwenye shule za ufundi wakatabasamu kwa furaha kama mzazi aliyepata salama.

Kwa miaka mingi, baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha wana wao. Hii ni kutokana na umaskini uliokithiri mipaka. Hali hiyo ilichangia huzuni kuu miongoni mwa familia. Pengo la waliosoma na wasiosoma lilizidi kuwa pana kielimu na kiuchumi. Uadui ukaingilia jamii. Ujambazi nao ukazidi.

Sasa watu wote wakipewa haki sawa ya kusoma, hata wale watoto wa maskini watamanio masomo watakinaisha kiu yao. Pia mengi ya matatizo yatapungua. Si kweli kuwa tajiri ni mwerevu kuliko mkata. Kila mwanajamii akipewa nafasi na asome kwa bidi atafua dafu maishani.

Vijana watakaofuzu katika shule za kiufundi wataweza kuajiriwa katika sekta mbalimbali. Mwishowe wakipata mtaji watajiendeleza kwa kuanzisha kwa miradi midogomidogo ya kujitegemea. Hali kama hii ikienea kote nchini viwanda vidogo vidogo vitaanzishwa na ajira itapatikana. Hiyo itakuwa njia mojawapo kuu ya kuuinua uchumi na kuzalisha nafasi nyingi za kazi. Kitaaluma, hawa vijana wataweza kuwa madaktari, wasanii, walimu......... na kazi nyingine nyingi. Kisomo ni kitamu. Hakifai kutiliwa nanga.

**41.** Uamuzi uliofanywa na serikali

A. ulisababisha kufurika kwa wanafunzi shuleni na kupita mtihani.

B. ulisababisha kuchipuka kwa vyuo vya ufundi na kuondoa umaskini

C. ulisababisha kuongezeka kwa watoto shuleni na kupata nafasi za kujiendeleza

D. ulisababisha kupungua kwa umaskini na kuwapa watoto nafasi ya kujiendeleza.

**42.** Baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha wana wao. Methali inayoafikiana na maneno haya ni?

A. Maskini kupata ni mwenye nguvu kupenda

B. Dau la mnyonge haliendi joshi

C. Ngombe wa maskini hazai pacha

D. Maskini halali mchana

**43.** Ukosefu wa elimu unasababisha

A. Umaskini, uadui, huzuni na ujambazi

B. Wivu, ujambazi, kukosa kiu ya kusoma na uadui

C. Utajiri, ukosefu wa kazi, huzuni na ujambazi

D. Ujambazi, wivu, utajiri, na kiu ya kusoma

**44.** Kulingana na kifungu, pengo kubwa la kiuchumi limesababishwa na nini?

A. Watoto kutopata kisomo kwa sababu ya umaskini

B. Uadui na ujambazi ulioikumba jamii maskini

C. Watoto kutopelekwa shule za kiufundi kutokana na umaskini

D. Wazazi kushindwa kupambana na umaskini

**45.** Ni kweli kuwa watoto wote wakipewa nafasi sawa

A. watoto wa maskini watakuwa werevu

B. watoto maskini na tajiri watakuwa sawa

C. watoto wote wapendao kusoma watakuwa matajiri

D. watoto wote wapendao kusoma watapata kisomo

**46.** Vijana wote wakipata mtaji

A. wataanzisha miradi ya kiufundi

B. wataweza hata kuwa wataalamu

C. wataanzisha shughuli za kujikimu

D. watakitilia kisomo chao makini

**47.** Kisomo hakifai kutiiwa nanga kwa kuwa

A. shule zitapanuka

B. kina manufaa mengi

C. serikali itakigharamia

D. watu watakuwa wataalamu

**48.** Neno kusajiliwa limetumika katika ufahamu. Lina maana gani?

A. Kurekebishwa

B. Kunufaishwa

C. Kuandikishwa

D. Kufundishwa

**49.** Hata wale maskini watakinaisha kiu yao ina maana kuwa

A. watapunguza tamaa yao

B. wataacha hofu yao

C. watafurahia hali yao

D. watatosheleza hamu yao

**50.** Kichwa mwafaka zaidi kwa taarifa hii ni

A. Ukarimu wa serikali

B. Kupunguza ujinga

C. Masomo ya kiufundi

D. Serikali kupanua masomo